



MIKONO YA USAIDIZI ULIMWENGUNI KOTE

KUTANA NA JAROM

kutoka Mexico

*Kutana na watoto wa Msingi
wakiwasaidia wengine, kama
Yesu alivyofanya.*



Yote kuhusu Jarom



LUGHA:
Kihispania

KUTOKA:
Jiji la Mexico,
Mexico

UMRI: miaka 10

6 Rafiki

MALENGO NA NDOTO:
1) Kuwa daktari wa mifugo au mwanaasaikolojia.
2) Kuchora picha nzuri.
3) Kuwatendea wengine kwa heshima na wema.




FAMILIA:
Jarom, Mama,
Baba, kaka wawili

VIELEZO NA MIKE LAUGHHEAD

Mikono ya Kusaidia ya Jarom

Jaromu ana mbwa watatu. Moja ya kazi yake ni kuwalisha kila siku. Anawapenda sana. Jarom pia ni msikilizaji mzuri na mmisionari. Alipojua kwamba babu wa rafiki yake alifariki, Jarom alimwita rafiki yake. Jarom alimsikiliza rafikiye. Pia alimfariji na kumwambia kuhusu mpango wa Baba wa Mbinguni kwa ajili yetu.

Jaromu anataka marafiki zake wawe na furaha. Mara nyingi anazungumza nao kuhusu Kanisa na kuwaalika kwenye mikutano na shughuli. "Unapoomba, kumbuka marafiki na familia yako," Jarom anasema. "Uliza kujua jinsi unavyoweza kuwasaidia." ●



Jarom humfuata Yesu kwa kuwfariji wengine. Fungua ukurasa ili kusoma hadithi kuhusu jinsi Yesu alivyotuhidi faraja.

Mambo Pendwa ya Jarom



HADITHI KUHUSU YESU:
Pale Yesu lipomsaidia kipofu na wakati alipofufuka.



SEHEMU:
Hifadhini na kanisani



WIMBO WA MSINGI:
"When I Am Baptized" (Kitabu cha Nyimbo za Watoto, 103)



VYAKULA:
Supu ya pozole,
chipsi na donati



RANGI:
Bluu na zambarau



MASOMO SHULENI:
Historia na jiografia

Jiunge na Timu ya Mikono ya Usaidizi!



Unapowahudumia wengine, wewe unakuwa sehemu ya Timu ya Mikono ya Usaidizi! Je, wewe unaweza kumhudumia nani?